

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**Verbatim Report Of**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MAKUENI  
CONSTITUENCY, HELD AT MAKUENI AIC WOTE**

**ON**

**11<sup>TH</sup> OCTOBER 2002**

**final copy**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MAKUENI CONSTITUENCY, HELD AT AIC WOTE  
ON 11<sup>TH</sup> OCTOBER 2002**

**Present**

Com. Abida Ali Aroni

**Secretariate in Attendance**

1. Collins Mukewa - Programme Officer
2. Susan Mutile - Verbatim Recorder

**3Cs Members**

1. Rose Mulu
2. Benard Maingi

The meeting started with Com. Abida Ali in the chair.

**Sammy Kiteng'u:** So, I want us to start of today's meeting by a word of prayer from Reverend Mulatya.

**Rev. Mulatya:** Okay na nitawasalimia kwanza. Hamjambo? Basi tuombe: Baba tunakushukuru sana kwa kuwa wewe ni Mungu mwena. Tunakushuru kwa kuwa wewe ni Mungu wa mipango na wewe ni Mungu wa mapenzi makuu. Na tunataka kujipeana mikononi mwako, hasa wakati huu tunapoketi hapa na kutafakari mambo makubwa yanayo husu nchi yetu. Leo kuna mazungumzo kuhusu Katiba mpya ambayo ni pendekezo nzuri la kuongoza watu wako. Hakuna jamhuri inayoishi vizuri, pasipokuwa na Katiba nzuri. Tunajua wewe ulipotaka kanisa lako lisisimame vizuri ulitengeneza ukaketi chini ukaandika Biblia

ambayo kwa kweli ndio Katiba ya wale ambao wanataka kuja kwako. Na tukitaka kwenda vizuri na muongozo mzuri tunasoma neno lako.

Ndiposa leo tunakusanyika hapa kwa kikao kingine, maana hiki sio kikao cha kwanza tumekwisha kaa kikao kingine. Yatakayo zungumzwa leo, viongozi wote watakao zungumza na wenye kuadhaa shughuli hii na mipango yote tunataka uwe pamoja nasi. Vile vile hatuwezi kusahau kumuomba kiongozi wa Commission hii, Professor Ghai ambaye anashika kazi ngumu na ma-Commissioner ambao wahudumu na yeye. Tunajua hii ni kazi ambao ikiisha itaongoza nchi hii miaka mingi na hata sio wakati mfupi. Labda itakwisha Yesu Kristo atakaporudi. Tunatake kuiweka katika misingi mizuri, misingi ya kufuatwa na yenye maadili mema yanayofaa wananchi watukufu. Tuongoze katika sherehe zote, shughuli zote, tukimaliza tutakushukuru. Katika jina la Yesu Kristo tunaomba na kuamini. Amen.

**Sammy Kiteng'u:** Tukianza, I would like to introduce to you the people who have made possible this day, and they are the 3Cs wa huku Makueni Constituency. Tuko na Rose Mulu na Benard Maingi. As we continue may be towards the end of the meeting, I will tell you the representatives that were elected by the county council Councillors. Now, without wasting more time let me give the mike to the Commissioner to introduce the people that she has come with from the head office. Thank you.

**Com. Abida Ali:** Hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Sammy Kiteng'u:** Sorry I had forgotten, my name is Sammy Kiteng'u. I am the district coordinator CKRC Makueni district. Thank you.

**Com. Abida Ali:** Hamjambo?

**Audience:** Hatujambo

**Com. Abida Ali:** Mimi naitwa Abida Ali Aroni naibu wa mwenyekiti wa Tume ya Marekebisho ya Katiba na leo nimeandama na Programme Officer Collins Mukewa na Verbatim Recorder Susan Mutile. Tutaanza nafikiri shughuli ya leo ingawa tunasikitika sana kwamba watu wachache sana wamejitokeza. Tulidhania kwamba hii sehemu yenu ya Makueni tungepata watu wengi zaidi kwa sababu tuko karibu na town, lakini tunatumaini kwamba watazidi kufika. Na wale mko hapa mtatusaidia kwa kuweza kueneza mambo ambayo tutaweza kuyazungumzia kwa siku ya leo.

Kwenya programme ya leo, nitawaeleza kwa kifupi ni kwa nini tumeandaa huu mkutano wa leo. Nitawaeleza pia jinsi ambavyo tuliweza kufanya kazi hadi tukafikia wakati huu wa kuweza kusabaza hii draft Constitution. Halafu, nitaweza kuwapeleka kupitia

kwa hiyo draft Constitution kwa kifupi sana halafu nitawapa nafasi ya kuweza kujadiliana au kuuliza maswali ikiwa kuna vifungu fulani ambavyo hamjavielewa.

Madhumuni ya mkutano huu wa leo, ni kutuwezesha kuwaletea rasmi draft Constitution ambayo mumeweza kupewa pale mlangoni. Kwa sababu ningetaka sana muweze kusoma kuelewa na muweze kujadiliana ili muwatume wale wakilishi watatu wa district yenu ambao watakuja katika kikao cha kitaifa. Muwatume, muwaeleze mambo ambayo mngetaka kuona katika Katiba mpya ikiwa mumefurahia hii draft Constitution mutaweza kuwatuma hili waje na kujidhinisha Katiba hii mpya. Ikiwa kuna mambo fulani ambayo mnadhandia yanafaa kuongezwa ama kubadilishwa, mtaweza kuwatuma ili katika huo mjadala wa kikao cha kitaifa mambo hayo ambayo mtaona ni muhimu yaweze kuongezwa ama kubadilishwa wakati wa kikao hicho ambacho ni kikao muhimu sana katika vikao vyote vya marekebisha ya Katiba.

Tulipokuwa hapa kuchukua maoni tuliwaeleza kwamba tungeweza kurudi na report za Constituency katika province. Lakini tulipomaliza shughuli za kuchukua maoni Bunge ikabadilisha sheria na ikawa sana hatutapata nafasi ya kuja katika province na kujadiliana report yenu, kwa sababu kama mnavyojua kuna watu wengi ambao wanahimiza kwamba Katiba mpya itoke haraka iwezekanavyo. Kwa hivyo pia ikapunguzwa muda wa kujadiliana na kwa wakati huu tuna kama wiki mbili, kujadiliana report hii kwa sababu hicho kikao cha kitaifa kinaweza kufanyika kuanzia tarehe ishirini na nane wa mwezi huu wa kumi.

Baada ya sisi kuchukua maoni yenu, na maoni ya Wakenya wote. Wakati ambapo tulizinguka katika Constituency zote za nchi yetu. Tuliweza kuandika watu ambao walitusaida katika kuchambua maoni yenu, na sisi tukaweza kusoma maoni hayo na pia tukaweza kuangalia report ambazo tulipewa na wataalamu kupitia washa ama workshop ambazo tulifanya pamoja na wataalamu tofauti wa hapa nchini na wengine ambao walitoka ng'ambo ili watusaidie kuelewa mambo tofauti tofauti ambayo mliyatajia. Baada ya kusoma ripoti hizo za wataalamu na kuangalia maoni yenu, tuliweza kuandika ripoti ambayo imesambazwa pia kupitia katika magazeti na nina hakika Bwana coordinator hana zingine ambazo pengine anaweza kuwapatia. Ambapo tumefupisha maoni ya wananchi katika ripoti ingawa tutatoa pia ripoti ambayo itakuwa ni ndefu na ina mambo mengi zaidi. Lakini kwa sababu ya wakati tumefupisha na kutoa ripoti fupi ambayo ilituwezesha na sisi kuweza kuandika hii draft Constitution, kupitia mambo ambayo mlitueleza. Na wakati kabla hatujaandika hii draft Constitution, kama Tume tuliweza kujadiliana kwa muda wa wiki mbili na hatimaye tukakubaliana kuwa ni hii draft Constitution. Na katika kuandika hii draft Constitution tulipitia njia tatu.

Kwanza, katika hizi chapters ama vifungu tofauti tulijadiliana na kuona kama sote tumekubaliana kwa kauli moja, na ikiwa tulikubaliana kwa kauli moja kukuwa hakuna shida. Wakati ambapo tulikuwa hatukubaliana tuliweza kutumia consensus. Consensus ni kusema kwamba tulijadiliana tukashauriana na hatimaye kukawa hakuna haja ya kupiga kura tukachukua kauli ambayo ilikuwa ni ya watu wengi. Kwa sababu pia katika sheria ambayo inahusishwa kazi hii ikiwa Tume haikubaliani wote, tunaweza kupiga kura. Lakini kukawa hakuna haja ya kura, tukatumia njia ya consensus kufikia mambo ambayo yako katika draft Constitution. Na kwa wakati huu tukaileta ilivyo ili muweze kuisoma. Kuna wale wanaona kwamba ni maneno mazuri na

hayafai kubadilishwa, kuna wengine wanaona kwamba kuna seheni kadhaa ambazo zinataka kubadilishwa. Kwa hivyo sasa ni jukumu lenu kusoma na kuhakikisha kwamba mambo yale ambayo yako hapo ni mambo ambayo yanafaa katika utawala wa nchi yetu kwa siku za usoni.

Kufikia hapo, nadhania sasa ingekewa bora tuangalie vifungu tofauti vya Katiba au proposal hiyo yetu, na ikiwa mna mambo ambayo hamjalewa au kuna mambo mngetaka niwaeleze kwa kirefu tuweze kufanya hivyo. Tunatarajia pia kwamba mliweza kusoma hapo mbeleni kwa sababu tulizitoa katika gaziti kama sasa nafikiri zaidi ya wiki mbili. Na mambo ni hayo hayo ambayo yalikuwa kwenye gazeti hayajabadilika. Na kwale ambao hawajasoma tungewaomba mzidi kusoma, na kujaribu kuwatuma hao watu watatu ambao mmewachagua kutoka katika district. Na pia, MP wa area yenu atakuwa ni delegate ikiwa kuna maneno ambayo mngetaka kumtuma, itakuwa pia ni sawa kumtuma katika National Conference.

Kwanza kabisa, katika hii draft tuna utangulizi au preamble kama mliyvyo tueleza, na pia tukaelezwa na Wakenya wengine kwamba kuna umuhimu wa kuwa na utangulizi ambao unatutambua sisi kama Wananchi wa Kenya. Kutambua tofauti zetu za kidini, za kimila na pia tutambue amani na haki ambayo tungetaka kuona katika nchi. Pia, mkatueleza kwamba mngetaka tutambue familia na jamii tofauti. Mkata pia tutambue haki na juhudi inayofanywa na akina mama na wanaume katika kukuza demokrasia na shughuli tofauti na sheria katika nchi yetu. Na pia mkata tusisitize kwamba nchi yetu ni nchi ya demokrasia ambapo wananchi wa kawaida wanapewa nafasi ya kujishughulisha na utawala. Sasa mtaangalia hiyo preamble ama utangulizi muone kama tumeandika mliyvyo taka ama mngetaka tubadilishe na kuongeza mambo fulani.

Katika chapter ya kwanza ya Katiba, tumeangalia umuhimu wa wananchi wa Kenya na tukapendekeza kwamba nguvu zote za jamhuri ya Kenya zimetokana na wananchi na ni lazima katika utawala wananchi wawekwe mbele. Na pia tukasema kwamba, nguvu hizi za wananchi zitapewa vyombo tofauti vya serikali. Vyombo hivyo kama mnavyo elewa ni Parliament. Na tukasema kwamba wanaokwenda katika Parliament, tumewapatia jukumu la kutuwakilisha pale. Tukasema pia, tumetoa nguvu zetu zingine au uwezo wetu tukaupa serikali kuu na kwamba watu ambao wamepewa jukumu la kuwa na kazi katika serikali kuu, watakuwa wanafanya kazi zao kulingana na Katiba. Tukasema pia tumetoa nguvu zetu zingine tukazipatia mahakama na kwamba mahakama hayo yanafaa kuwa ni huru na litafanya juhudi zake zikiwa zinaweka matumaini yetu kama Wakenya mbele. Halafu, tukawa na vyombo vingine ambavyo tunaita ni vyombo vya Kikatiba ambavyo tutavipatia uwezo na tunatarajia kwamba vitafanya kazi kulingana na vile ambavyo vitapewa nguvu na Katiba ya nchi yetu.

Katika section ya pili ama Article au kifungu cha pili tumetambua umuhimu wa Katiba katika nchi. Halafu, kifungu cha tatu tumeeleza jinsi ambavyo tunaweza kuhakikisha kwamba mambo yetu ya Kikatiba yanatimizwa. Na tumesema jambo ambalo halikuwa, tumependekeza jambo ambalo halikuwa katika Katiba iliyopita. Na tukasema mtu yoyote anaweza kupendekeza kesi katika korti wakati ambapo anaona kuna jambo ambalo ni la Kikatiba limekosewa. Na kwamba korti itaweza kutoa amri inayofaa kuhakikisha kwamba Katiba yetu imewajibika. Na katika Article ya nne, tumesema kwamba serikali yoyote itakayo jaribu kufanya kazi kinyume cha sheria itakuwa haifanyi kazi ambayo inafaa na kazi ambayo ni ya halali.

Katika kifungu cha tano, tumeangalia sheria za Kenya na tukazifafanua kuliko vile zilivyokuwa katika Katiba ya hapo mbeleni. Tumependekeza kwamba sheria kuu ibaki ikiwa ni hii Katiba ya nchi yetu. Tukapendekeza kwamba ifuatiwe na sheria ambazo zimetungwa na Parliament, kwa sababu hii Katiba tumetunga sisi kama wananchi lakini sheria zitakazo tungwa na waakilishi ziwe chini ya Katiba. Tumependekeza kwamba sheria pia za kitamaduni ziweze kutumika kama sheria za Kenya. Tumependekeza pia sheria ya jamii ya Kiislam na ya Kihindu. Na pia tukapendekeza kwamba sheria ambazo hazijaandikwa lakini zimetumika na zikawa ni kama desturi ambazo kwa Kiingereza zinaitwa common law, pia zitumike wakati ambapo kutakuwa na haka yake. Tumependekeza kwamba sheria zitakazo tungwa na jumuhia ya Afrika ya mashariki pia zitumike. Na pia sheria au utaratibu utakao wekwa na nchi zingine za ulimwengu ziwe zinatumika kama sheria ya nchi yetu.

Halafu katika chapter ya pili, tumeangalia kama jamhuri ya Kenya tutaishi na kufanya mambo kwa njia gani. Na kwanza kabisa tumetambua mambo ambayo pengine ni muhimu katika jamhuri. Na tumesema kwamba jamhuri yetu ya Kenya iwe ina malengo ya kitawala ambayo tutakuwa na utawala bora wa viama vingi. Utawala wa kidemokrasia na utawala utakao husisha wananchi wa kawaida. Tumesema tuwe na uwazi na uwajibikishaji katika utawala huo. Tuwe tuna vyombo vya kiserikali ambavyo vina mipaka na ni huru. Tuwe ni jamhuri ambayo inazingatia sheria, inazingatia haki za kibinadamu na uhuru wa mtu binafsi. Tukaangalia mipaka tofauti ya nchi yetu, katika schedule mkiangalia upande wa nyuma wa hiyo karatasi ambayo mnayo.

Katika schedule ya kwanza, mtaona tumeandika mipaka tofauti yetu ya Kenya na majirani kwa mfano Kenya-Uganda, Kenya-Tanzania, Kenya-Ethiopia, Kenya-Sudan, Kenya-Somalia. Tumeandika kwa urefu baada ya kuzungumza na wataalamu wa mambo haya. Tumeangalia pia miji tofauti na tukapendekeza kwamba Nairobi ibakie ndio mji mkuu na kwamba Bunge itoe sheria itakayo simamia mji mkuu. Na pia tukapendekeza kwamba, mikataba ni misimamo tofauti ya kiserikali isabazwe katika sehemu zingine za nchi ambazo tutakuwa na utawala wa mashinani.

Tukatanzama pia na kupendekeza kwamba tuwe na lugha ambayo ni lugha rasmi na tukapendekeza kwamba Kiingereza na Kiswahili ziwe ndizo lugha rasmi na kukiwa na mambo yote ambayo yamechapishwa kwa Kiingereza ni mpaka yaandikwe kwa lugha rasmi ambayo ni lugha ya Kiswahili. Na pengine kufikia hapo ningeomba msamaha kwamba hii draft Constitution ambayo tumewaletea hiko katika lugha ya Kiingereza ingawa tungewaletea pia ya lugha ya Kiswahili lakini pengine baada ya siku chache Bwana coordinator ataletewa ambazo zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Tuliziwacha zikichapishwa na kwa sababu ya haraka ambayo tunayo kumaliza shughuli hii ikawa hatukuweza kuzisubiri ili ziletwe kwa wakati huu. Lakini pengine kufikia wiki ijayo atapata nakala ambazo zimeandikwa kwa Kiswahili. Na pia tukesema kwamba ingawa Kiswahili ni lugha rasmi pia iwe ni lugha ya taifa. Na tukapendekeza kwamba lugha zote za nchi ya Kenya, pamoja na lugha inayotumika kwa watu wasio jiweza kwa mfano lugha ya ishara na pia Braille, ziweze kukuzwa kama vitu ambavyo ni muhimu.

Tukazatama serikali na dini, na tukapendekeza kwamba kusiwe na dini yoyote ambayo inasemekana ndio dini rasmi ya nchi yetu. Kwamba tuwe na tofauti baina ya serikali na dini na kwamba dini zote ambazo tunaziabudu katika nchi hii ziwe zinachukuliwa na kupewa uzito wa usawa. Tukatazama vyomba ambavyo tunatambua ni vyombo muhimu na vyombo ambavyo

ni vya kitaifa. Tukapendekeza kwamba bendera ya Kenya iwe ni chombo kimoja cha kitaifa na pia national anthem au wimbo wa taifa. Tukapendekeza pia court of arms ama muhuri ambao unatumika katika chapa ambayo unaona katika vitu ambavyo ni vya kiserikali. Na pia tukasema muhuri rasmi wa nchi yetu pia uwe unatambulika kama chombo cha kitaifa. Tukatambua pia katika kifungu cha tatu siku ambazo ni za kitaifa na tukatambua siku tatu peke yake. Na tukapendekeza zile zingine ziondolewe tubakie na tarehe moja mwezi wa sita Madaraka day, December tarehe kumi na mbili Jamhuri day na tumependekeza kwamba tuwe na siku ambayo tutaidhinisha Katiba hii kwamba ifanywe ni siku ambayo ni ya kitaifa. Kuna wale wanadhania kwamba hilo sio jambo nzuri na kuna siku zingine za kitaifa tumeziwacha sasa tungependa kufuata maoni yenu kuhusu jambo kama hilo.

Katika chapter ya tatu, tunaangalia National Goals and Values and Principles au maadili ambayo yatatuwezesha kuendesha nchi yetu na maadili ambayo ni muhimu katika kuendesha shughuli zetu kama Wakenya. Na mambo ambayo tumetambua kama maadili ya nchi yetu ni uhuru wa mwananchi, umoja wa taifa letu, usawa na udhamini wa jamii, demokrasia na utawala mwema na utawala wa kisheria. Tumependekeza pia haki za kibinadamu, usawa wa watu wote bila kuangalia jinsia yao. Tumependekeza bidii ya wananchi hili kufanikisha mahitaji ya kimsingi. Tumependekeza pia ushiriki wa watu binafsi katika shughuli za umma. Uhadhilifu wa kibinafsi na wa kitaifa. Pia tumependekeza uvumilifu na kutoa heshima kwa maoni ya watu wengine. pia tumependekeza mila na maadili tofauti ya jamii za Kenya. Tumependekeza pia kuleta utawala karibu na wananchi. Utatuzi wa mabishano kwa njia ya amani na pia jinsi tutakavyo kuza taifa letu liwe ni miongoni mwa utaifa na umoja wa nchi za Afrika. Mengine mtaweza kusoma nimewapatia kwa kifupi sana. Tumependekeza pia katika sehemu hiyo jinsi ambavyo vyombo au shirika zizizo za kiserikali zitaweza kupatiwa nafasi katika utawala wa nchi.

Katika chapter ya nne, tumeangalia uraia na kwa kifupi sana nitawaeleza mapendekezo ambayo tumeyatoa na tumesema kwamba kuna njia tofauti za mtu kupata uraia wa Kenya. Na tumependekeza kwamba iwe ni kwa kuzaliwa na kwa kujiandisha na pia kwa kuidhinishwa kuwa mwananchi wa Kenya. Tumependekeza pia umoja na usawa wa haki zote kwa kila mmoja ambayo ni mwananchi wa Kenya. Tumesema pia katika majukumu ya kiraia kuwe na usawa na pia katika kutoa vitambulisho ama passport kuwa na usawa kwa wananchi wa Kenya bila kubagua watu kupitia rangi yao, dini au kabila lao. Na pia tukependekeza kwamba, mtoto yoyote chini ya miaka minane ambayo atakayepatikana katika nchi yetu na hawezi kujitambua kupitia kwa wazazi aweze kupewa uraia wa Kenya. Tumependekeza pia kwamba raia wa Kenya aweze kupata uraia wa nchi nyingini kwa kimombo dual citizenship. Na pia tumependekeza kwamba kuwa kumewekwa boards au watu watakao simamia uwadhibishaji wa uraia kwa watu ambao watapendekeza kutaka uraia wa Kenya.

Na katika chapter ya tano ambayo ni muhimu zaidi tumeangalia haki za kimsingi au haki za kibinadamu. Na nitawapitisha kwa haraka na nyinyi mtazidi kusoma na kuona kama kuna haki zozote ambazo zimebakia ama mmependezwa na mambo ambayo tumeyaandika. Na katika sehemu hiyo kuanzia utaona ina vifungu vingi tumeanzia ishirini na tisa, hadi kifungu cha sabini na tano.

Na tukasema kwamba haki za kimsingi ni muhimu katika uendeshaji wa nchi ambayo inazingatia demokrasia. Tukapendekeza kwamba, hizi haki zipewe kila Mkenya bila ubaguzi wowote na tukapendekeza kwamba serikali iwe na jukumu la kuweza kutoa haki hizi. Na katika kigungu thelathini tumeeleza haki ambazo ni lazima zifuatwe na serikali.

Na katika kifungu thelathini na moja tumesema kwamba, ingawa tuna hizi haki wakati wingine haki hizi zitaweza kupunguzwa hili tusiweze kuingiliana na kuharibu haki za watu wengine. Na ukiangalia kifungu cha thelathini na mbili tumesema kwamba kila Mkenya hana haki ya maisha, right to life. Na ikiwa kila mwananchi hana haki ya maisha tumependekeza basi hukumu ya kifo iondolewe. Halafu tukaangalia usawa katika hizi haki na tukasema usawa huu uwezi kuwa kwa kila Mwanakenya na sheria iweko ili kuweze kusimamia hizi haki. Tukapendekeza kuwa kuwe na haki ya kutobaguliwa na tukasema hakuna Mkenya atakaye baguliwa kwa sababu ya rangi, umbo lake au msimamo wake katika jamii, kabila lake, umri wake, kwa sababu ni mlemavu, kwa sababu ya lugha yake ama jinsi alivyo zaliwa.

Tukaangalia haki za wanawake katika kifungu thelathini na tano, tukasema kwamba wana haki ya kupewe usawa na wanaume hasa katika shughuli za uchumi, shughuli za kijamii na siasa. Tukasema kwamba wanawake pia wapewe heshima kama wanavyo pewa wanaume na wapewa haki sawa katika urishi wa mali katika umiliki wa mali na kuweza kujishughulisha na shughuli ambazo ni za kiuchumi. Na tukapendekeza kwamba kusiwe na sheira yoyote, iwe ni ya kitamaduni, iwe ni ya kimila itakayo mbagua na kukosa kumpatia mwanamke usawa katika mambo yake. Na tukapendekeza kwamba ni jukumu la serikali kuhakikisha kwamba wanawake wametambulika hasa katika shughuli zao za uzazi na wamepewa nafasi na usaidizi utakao wawezesha kuendesha mambo yao. Pia tumependekeza haki za watu wazima na tukapendekeza kwamba ni jukumu la familia ya watu hawa wazee pamoja na serikali kuweza kuwawezesha kufanya mambo yao, kuwapatia heshima, kuwapatia nafasi ya kujiendesha na pia kuwapatia reasonable care and assistance au kuhakikisha kwamba wameangaliwa kwa njia inayostahili.

Pia tukapendekeza haki ambazo tunasema ni haki za watoto. Na tumependekeza kwamba watoto wote wanao zaliwa katika ndoa ama nje ya ndoa waweze kupatiwa usawa wa sheria. Na kwamba jambo lolote litakalo fanyiwa mtoto lifanyiwe mtoto huyu ikiwa tumeweka masilahi yake mbele. Pia tumependekeza kwamba wazazi wote wawili waweze kumuangalia huyo mtoto na wamepewa jukumu sawa kisheria.

Halafu tumependekeza sehemu ya familia katika nchi yetu, na tukasema kwamba mtu yoyote ambaye amefikisha umri wa miaka kumi na nane apatiwe nafasi ya kuoia ama kuolewa na kuweza kuunda familia. Na kwamba katika ndoa bibi na bwana tumependekeza kwamba wawe na haki sawa na hata watakapo kuwa kumewachana wawe na haki sawa katika shughuli zao. Na kwamba sheria itambue ndoa za kidini na ndoa ambazo zitakuwa zimefanywa kupitia taratibu za kimila.

Tukaangalia pia haki za watu walemavu na tukapendekeza kwamba serikali itoe utaratibu atakao tambua haki za watu walemavu. Tukapendekeza kwamba wapewe elimu na vifaa vya elimu vya kutosha. Na tukapendekeza kwamba serikali ihakikishe kwamba vyombo vya usalama na nyumba zote ambazo ni za kiserikali zitakuwa na vifaa zitakavyo wezesha watu hawa kuweza kutumia vifaa hivyo. Tukapendekeza kwamba serikali itambue na kukuza lugha ya ishara pamoja na Braille ili watu wasio jiweza au walemavu waweze pia kuelewa mambo ambayo yanafanyika. Na kwamba watu walemavu waweze kuhuzishwa katika sehemu zote za utawala.



Pia katika hizi haki za kibinadamu tumezungumzia kuhusu haki za kisiasa, haki ya kuweza kutembea na kuishi pahali popote katika nchi ya Kenya. Haki ya mtu kuweza kufanya kazi au biashara anayotaka. Tumependekeza pia haki za wafanyikazi. Tumependekeza kwamba serikali itoe huduma kwa watu ambao wasio jiweza kabisa. Tumependekeza kwamba kila Mkenya apate nafasi ya kuweze kuishi katika nyumba inayofaa. Tumependekeza kwamba kila Mkenya aweze kupata chakula na kutoweze kukaa njaa. Tumependekeza kwamba kila Mkenya aweze kuhudumiwa na kupewa maji masafi na maji yaliyotosha. Tumependekeza haki za wanunuzi wa huduma na vifaa. Pia tumependekeza haki ya kila Mkenya kuweza kufika katika mahakama na kuhudumiwa kwa njia iliyo bora na kwa haraka. Tumependekeza pia kwamba watu wanaoshikwa na kupelekwa katika cell za polisi, wasiwekwe kupita masaa arubaini na nane. Haki ya elimu na tumependekeza kwamba serikali itoe elimu ya kimsingi na ya lazima kwa watoto wote.

Katika chapter ya sita, tumezungumzia haki ya uwakilishaji ambapo tumeangalia mambo yanayo husika na upigaji wa kura. Na tumeangalia hapo kuanzia kifungu sabini na sita. Na tumependekeza kwamba ni haki ya kila Mkenya kusimama kwa kutaka kura na kupiga kura. Tumependekeza kwamba kura iwe ni ya siri na kwamba upigaji kura uwe ni wa haki na wa halali. Na kwamba tutakapokuwa tunapiga kura, tutahakikishiwa kwamba matokeo ya kura hizo zitakuwa ni matokeo ambayo ni ya haki. Na kwamba katika upigaji wa kura wanawake, watu walemavu na jamii ambazo zimetengwa zitapewa nafasi. Na katika haki ya kupiga kura tumependekeza kwamba iwe ni lazima kila Mkenya ambayo amefikisha umri wa miaka kumi na minane kupiga kura. Tumependekeza ni akina nani watakao weza kujiandikisha na ni vipi mtu atakosa kuandikishwa kama mpiga kura. Tumependekeza pia hili Tume la kupiga kura na tukapendekeza kwamba Tume hii ipuguzwe wanachama kutoka watu ishirini na mbili wapuguzwe ni watu wasio pugua nane na wasio zidi watu kumi.

Tukapendekeza pia shughuli za Tume hii na tukaweza kupanua shughuli zake. Tumesema kwamba, Tume hii ama tumependekeza kwamba Tume iwe inaandikisha wapiga kura kila wakati. Tumependekeza kwamba Tume hii pia, iwe na kazi ya kusimamia shughuli za kupiga kura na kwamba pia katika kazi yake iwe ni kuhakikisha kura zilizo za haki na za halali. Pia isimamie vyama vya kisiasa, isimamie pesa zitakazotolewa na serikali kwa vyama vya kisiasa kwa sababu tumependekeza kwamba pesa fulani katika budget ya nchi zipewe vyama vya kisiasa. Tumependekeza kwamba zisimamie mizozo yoyote itakayo kuwepo wakati wa kupiga kura na kwamba wasabaze elimu ya upigaji kura na demokrasia. Na pia watazame maneno ambayo ni ya Constituencies na mipaka ya Constituency. Na watakapo zungumza na wananchi ili kuona jinsi watakavyo panua ama kuangalia mipaka, watazame wananchi au population ya Constituency, waangalie jiografia ya Constituency, waangalia haja za jamii inayoishi pale na waangalie census ama ripoti ambayo ilitolewa baada ya kufanyiwa hesabu. Na kazi hii wale wanafanya baada ya miaka kumi.

Pia tumeangalia na kupendekeza mambo mengi kuhusu vyama vya kisiasa na jinsi shughuli zao zitakavyokuwa zinaendeshwa. Na tukapendekeza kwamba kila Mkenya awe na haki ya kuunda chama cha kisiasa au kujiunga na chama cha kisiasa. Tumependekeza pia jinsi vyama vya kisiasa vitakuwa vinaendesha shughuli zake na tukasema kwamba bali na kujishughulisha

na upiga kura kwamba vyama vya kisiasa viweze kueneza mambo tofauti kama vile elimu ya demokrasia, viweze kusimamia shughuli za serikali kuhakikisha kwamba kuna uwazi na uwajibikishaji wa shughuli hizi za serikali. Na tukasema kwamba au tukapendekeza kwamba 0.3% ya budget ya nchi yetu itengwe ili kuhudimia vyama vya kisiasa. Na tukapendekeza kwamba asilimia hamsini ya pesa zitakazo tengwa zipewe vyama vyote vitakavyoweza kupata asilima tano ya kura zitakazokuwa zimepigwa nchini. Halafu zile zingine zitabakia zingawanyishiwe vyama vya kisiasa kulingana na viti ambavyo watakuwa wamevipata. Na tukapendekeza kuwe na nidhami katika hivi vyama vya kisiasa. Na kwamba vikikosa kufuata utaratibu fulani, vinaweza kutolewa na kufutiliwa mbali.

Katika chapter ya saba tunaangalia na kupendekeza Parliament ama Bunge na hii tumependekeza katika ukurasa mia moja na moja, 101. Tumependekeza kwamba tuwe na Bunge itakayo kuwa na sehemu mbili. Tumependekeza National Council ama Senate au Upper House na tukapendekeza National Assembly au Lower House. Na tukapendekeza kwamba njia ya uchaguzi iwe ni tofauti kwamba watakao enda katika hiyo nyuma ya juu Upper House, wawe wamechaguliwa kutoka katika district tofauti. Na watu ambao watakuwa katika (end of side A)-- vitengwe kwa akina mama na hawa wachaguliwa kutoka katika kila province. Na kila province ichague akina mama wanne na hio sasa kwa vile tumetambua province saba, watakao salia watatoka katika mkoa wa Nairobi kwa sababu Nairobi ni mkoa na pia ni district. Na hawa watu watachaguliwa kupitia kupiga kura.

Katika hiki chumba cha pili ama National Assembly, tumependekeza kwamba tupige kura za Wabunge mia mbili na kumi kama kawaida, kupitia kura kama tunavyofanya kawaida. Halafu tumependekeza kwamba, kuwe na wanachama mia tatu. Kwa hivyo tutakuwa tumebakisha viti tisaini na tunapendekeza. Kwamba, viti hivi vipewe watu watakao tolewa katika ordha zitakazo tolewa na vyama party list.

Kwamba vyama ambavyo vitakuwa vimewasilishwa Bungeni, vitatoa orodha ya majina kulingana na watu ambao wangetaka wateuliwe katika Bunge. Na tumependekeza kwamba hiyo orodha itoe majina ifuatayo.

Ikiwa mtu wa kwanza ni mwanamke wa pili awe ni mwanaume na hivyo hivyo mpaka kufikia number itakayo tolewa na Tume hii ya kupiga kura. Kwa hivyo tunapendekeza kwamba tuwe na Parliament itakayokuwa na Wajumbe mia nne.

Halafu tunapendekeza kwamba Ministers na Deputy Minister wawe ni kuma na watano na watoke nje ya Bunge wasiwe ni watu ambao tumewatuma kule Bungeni. Pia, tumependekeza kwamba kikao cha Bunge kitakuwa ni Nairobi na kwamba Bunge litajiwekea calender yake na kwamba Bunge haliwezi kufutwa kabla ya kupitisha muda wake wa kazi. Na tumependekeza kwamba, National Council ama Upper House iwe inafanya kazi yake kwa miaka minne na National Assembly iwe inafanya kazi yake kwa muda wa miaka mitano. Na kwamba Bunge litakuwa na uwezo wa kuweza kupitisha kura ya kutokuwa na imani kwa Waziri Mkuu, kwa sababu tumependekeza kuwe na Waziri Mkuu.

Kisha tukiangalia serikali kuu, tulivyo pendekeza ni kwamba seriakali kuu iwe kuna Rais atakayekuwa amechaguliwa na wananchi wote. Huyu Rais awe amesimama pamoja na mtu tutakaye mchagua kama Makamu wa Rais. Kwamba kiti cha Makamu wa Rais akitapigiwa kura. Tukimchagua Rais, tutamchagua pamoja na mwenzake au running mate ambaye atakuwa ni Makamu wa Rais na atatakiwa awe na qualification ambazo zitakuwa ni sawa na zile Rais kwa sababu kuna wakati ambapo atasimama kama Rais wakati ambapo Rais atakuwa hayuko, atakuwa ni mgonjwa ama atakuwa amefariki.

Na pia tumependekeza kwamba kuwe na Waziri Mkuu na huyu Waziri Mkuu tumependekeza kwamba, achaguliwa apendekezwe kwa National Assembly au Lower House na Rais na kwamba ni lazima aidhinishwe na Bunge. Ikiwa Bunge limemkataa basi hawezi kuwa Waziri Mkuu ni lazima akubalike na Bunge na Rais atakapo mchagua huyu mtu kwamba kabisa tumependekeza kwamba awe ni kiongozi wa chama kitakacho kuwa na wakilishi wengi katika Bunge. Na ikiwa mtu huyu ambaye amependekezwa na Rais amekataliwa na akakosa kuidhinishwa na Bunge, basi mtu atakayekuwa anasimamia vyama vya upizani atapewa nafasi ya kupeana jina na ikiwa jina ambalo amepeana limekataliwa na Bunge basi Rais ataulzwa kuchagua Mbunge yoyote kuwa ndiye Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu atafanya kazi yake mpaka wakati atakapo fariki au wakati atakapofutwa kazi na Bunge kwa kupitisha kura ya kutokuwa na imani na yeye ama atajiuzulu. Na ikiwa hayo mambo hayajafanyika basi atafanya kazi mpaka wakati ambapo tutaenda kwa kura.

Katika serikali kuu, pia tumependekeza kwamba tuwe na Mawaziri kumi na watano na manaibu Deputy Ministers kumi na watano, watakao wasaidia hao Ma-ministers. Tumependekeza tabia ambayo itakayofuatwa na Baraza la Mawaziri. Tumependekeza kwamba pia kuwe na Tume itakayo angalia mishahara ya Rais, Makamu wa Rais, Mkuu wa Mawaziri na pia Mawaziri na Makamu wao. Na pengine pia tungependa kuangalia shughuli ambazo kwa kifupi zitakuwa zinafanywa na Rais na zile ambazo zitakuwa zinafanywa na Waziri Mkuu.

Kwanza, Rais anatakiwa kufanya mambo yafuatayo ambayo ni mambo ya kisiasa. Ni lazima alinde uhuru wa taifa, ni lazima aheshimu wingi wa kitaifa na ulinzi wa haki za kibinadamu na ni lazima alinde Katiba na atetee kanuni za sheria. Na pia katika sheria, jambo muhimu ni kwamba ni lazima sahihi ama idhini ya Rais iwe katika miswada yote au sheria au bill zozote zitakazopitishwa na Bunge. Naye Rais amepewa haki ya kuweza kupitisha ama kuidhinisha hizo sheria kwa mara moja, anaweza kukataa na kuridisha hiyo sheria kwa Bunge au anaweza kuomba korti kuu Supreme Court kuweza kumpatia mawaidha kuhusu pendekeza ambalo limepitishwa na Bunge kama mswada au bill ama sheria mpya.

Rais pia amepewa majukumu mengine, kwa mfano kama nilivyo waambia kutafuta ushauri wa korti kubwa. Pia amepewa jukumu la kuhutubia Bunge rasmi mara moja kwa mwaka ingawa anaweza kuhutubia Bunge kwa mara zingine akiona haja ya kufanya hivyo. Atahakikisha kwamba tumekuza demokrasia katika nchi yetu na tumefadhili na kutumia fedha za nchi kwa njia iliyo bora. Na pia anaweza kupendekeza hatua za kisheria kupitia kwa baraza la Mawaziri na sio direct. Na pia ni lazima Waziri

Mkuu, kila wakati kumueleza na kumfahamisha Rais shughuli za kitawala za nchi yetu. Rais pia amepewa uwezo ufuatao:-

Amepewa uwezo wa kuwa ndiye mkuu wa majeshi na anasimamia baraza la usalama wa kitaifa, National Security Council.

Aneweza kutangaza hali ya hatari baada ya kushauriana na Waziri Mkuu na Baraza na pia baada ya jambo hili kuidhinishwa na Bunge.

Anaweze pia kuteuwa Makakimu kulingana na pendekeza atakalo pata kutoka kwa Tume ya huduma za mahakama

Na pia anauwezo wa kuanzisha utaratibu wa kuwaondoa Mahakimu na Ma-judge.

Anaweza pia kuidhinisha makataba ambayo tumeweza kuingia na nchi za kingeni.

Anaweza kuwateuwa mabalozi na kupokea mabalozi watakaokuwa wametumwa na nchi zao. Na pia kuongoza wakati ambapo Bunge linapofungwa.

Naye Waziri Mkuu atakuwa ndiye msimamizi wa shughuli za kiserikali kwa sababu ndiye atakaye simamia Baraza la Mawaziri. Anatakuwa anapendekeza na kusimamia makadirio ya kifedha budget. Atawakagua na kuwapendekeza Mawaziri na pia Manaibu wa Mawaziri na yeye ndiye atapendekeza maswala ya kiserikali yote. Na pia kupendekeza miswaada ya kiserikali yote na ni lazima ahudhuri Bunge. Kwa vile tumeona sio lazima kwa Rais kuhudhuria Bunge.

Tumeangalia pia mahakama katika chapter ya tisa na tumependekeza kwamba tuongezewe tuongozewe korti nyingine itakayoitwa supreme court. Na itakayo simamiwa na ma-judge wapya, ambao hawafanyi kazi kwa wakati huu. Tumependekeza pia kuwe na hiyo Tume itakayo simamia huduma za mahakama za mahakama na tukaipatia kazi zaidi itakavyo weze kuchunga na kuhakikisha kwamba mahakama zinahudumia wananchi vilivyo. Tumependekeza watu watakao weza kuandikwa kama ma-judge na tumependekeza watafanya kazi yao hadi miaka migapi, tumependekeza kupuguza kutoka miaka sabini na miwili hadi miaka sitini na nne. Tumependekeza jinsi ambavyo Rais anaweza kuanzisha utaratibu wa kuondoa judge katika kazi yake kwa sababu hatungependa wafutwe kazi hivi hivi, kwa sababu itakuwa hawawezi kufanya kazi yao kwa njia ya uhuru na njia inayostahili.

Pia tumeangalia ofisi ya Mkuu wa Sheria, na tukapendekeza kwamba ofisi hiyo igawanyishwe mara mbili. Kwamba tuwe na atakayekuwa ni msimamizi wa shughuli za kiserikali, Legal Adviser ambaye tumependekeza ambaki na jina la Mkuu wa Sheria. Halafu tumesema kuwe na Director of Public Prosecution mtu atakaye kuwa anasimamia na kutetea kesi za kiserikali, ambaye kwa wakati huu ako chini ya Mkuu wa sheria lakini tumesema tugawanyishe na awe kazi yake ndio ya kuenda kortini.

Halafu kuna mtetezi wa haki za wananchi ambaye ni Public Defender ama kwa lugha nyingine ni Ombudsman, tumesema ofisi hiyo pia iwekwe ili wananchi wa kawaida wawe na pahali pa kuenda na kulalamika wakati ambapo wanadhulumiwa.

Pia tukaangalia shughuli za mawakili kwa sababu tumeonelea kwamba mawakili huwa kazi yao ni kulinda sheria na ingefaa mambo yao yawekwe katika Katiba. Na tumependekeza mwanzo kabisa kwamba shughuli zao ni kulinda na kutetea Katiba ya nchi yetu. Na pia shughuli yao ni kuweza kufanya kazi yao kwa njia iliyo bora na njia ya uhaminifu, wakiwa wameweka haki na haja za wateja wao. Na pia shughuli nyingine ni kwamba, mbali na kuweza kuharibu shughuli na haki za wateja wao wataweza kushughulika pamoja na mahakama kuhakikisha kwamba hukumu inayo tolewa ni hukumu ya haki.

Katika chapter ya kumi tumeangalia utawala na jinsi ambavyo utawala huo utaweza kufika hadi mashinani kama mlivyo tuagiza. Ukurasa mia mbili na kumi na tatu tumezungumzia mambo hayo. Tumependekeza kwamba utawala ugawanyishwe hadi mashinani ili kuhakikisha kwamba huko karibu na wananchi na kwamba wananchi wanajihuzisha pia tuweze kuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba kuna checks and balances. Na kwamba rasilmali za nchi zinaweza kugawanyishwa kwa usawa na pia tutaweza kupata huduma inayofaa kama wananchi na tukapendekeza kwamba utawala huu ugawanyishwe mara nne.

Kwamba utawala uanzie katika vijiji, ufike katika locationa ama kasa na ufike katika district hatimaye ufike katika province. Na tukaeleza jinsi ambavyo utawala huu utagawanyishwa na jinsi ambavyo watu watatawala kwa mfano, katika vijiji tumependekeza kwamba wazee wa vijiji wapewe nafasi ya kuwa ndio watawala au ikiwa haiwezekani kijiji kitakachokuwa hakina wazee wa kufanya kazi hiyo wachague viongozi wasiodizi kumi na wasio pugua sita. Katika kata ama location, tumependekeza kwamba representatives wawili watoke katika kila kijiji, katika location hiyo ili waweze kuunda location councils na katika hao viongozi wawili mmoja awe ni mama. Na kwamba watachagua ni nani atakayekuwa ni msimamizi ama administrator.

Tukitoka hapo tunaingia katika districts ama wilaya na tumependekeza kwamba, wilaya ndio iwe na nguvu zaidi katika hizi serikali za mashinani na kwamba watakao chaguliwa wawe ni watu ishirini na wasididi thelathini na wachaguliwe kupitia kura na pia msimamizi wao haweze kuchaguliwa na wananchi.

Halafu kutoka hapo tunaenda katika mikoa, na watu watakao kuja katika mikoa ni watakao toka katika wilaya watu wawili katika kila wilaya katika mkoa huo mmoja awe ni mama. Na tukasema kazi kubwa ya wilaya au serikali ya wilaya itakuwa, ni kukuza utawala katika district councils na kuwasaidia kuweza kupanga mipango yao ya utawala. Na tutatoa kwa kirefu sheria itakayo tumika katika utawala huo wa mashinani mtaweza kusoma.

Katika chapter ya kumi na moja tumezungumza kuhusu mashamba na mali. Tumependekeza kwamba serikali izidi kuangalia mipango na utaratibu wa mashamba. Tumependekeza kwamba serikali ijaribu kugawanya kwa usawa na kuwapatia watu nafasi ya usawa kufikia mashamba. Na kwamba watu ambao wana mashamba, mashamba yao na mali yao ilindwe na tuweze pia

kutumia shamba hizi na mali hii kwa njia ambayo inafaa. Tuweze pia kuifadhi udongo kwa njia inayofaa. Tukasema kwamba kila Mkenya aweze kumiliki ardhi sehemu yoyote ya nchi yetu, na kwamba mgeni asipewe nafasi ya kumiliki ardhi. Wawe wanakodi ardhi kwa miaka isiyopugua tisaini na tisa, sio kuwa ni wenye ardhi lakini wawe wanakodi. Na kwamba kuwe na umiliki wa ardhi wa aina tatu, wa binafsi wa jamii na wa jumhia, private, community na public land. Na tukapendekeza kwamba, mashamba yote ambayo sasa yanasemekana kwamba ni trust land yaweze kuandikwa majina na vikundi au jamii.

Tukapendekeza pia kuundwe Tume itakayo simamia shughuli za mashamba, Tume ambayo itahakikisha kwamba sheria zote ambazo zinasimamia mashamba zimeweza kutengezwa kwa sababu kwa wakati hazilingani na hazifanani. Na pia Tume hii itaweza kuwa ndio msimamizi wa mali au shamba la umma. Na pia Tume hii itaweza kuangalia jinsi ambavyo ubadilishanaji wa umilikiwa wa ardhi utarahisishwa kwa sababu kwa wakati huu kazi hii ni ngumu. Pia wataweza kutafuta suluhisho katika maadhibio ambayo ni ya kihistoria kwa jamii fulani fulani kuhusu umiliki wa ardhi. Kwa mfano, jamii ya watu wanaoishi mkoa wa Pwani wamelalamika wakisema wao ni ma-squatters katika mashamba ambayo ni ya mababu yao. Pia watu wa North Eastern malalamishi na pia watu wa Rift Valley na sehemu zingine pia sehemu za Eastern province mmelalamika sasa tumependekeza kwamba wasuluhishe mambo kama hayo.

Pia tumeagalia mazingara na jinsi ya kuweza kulinda mali asili matasoma na kuangalia tulivyo pendekeza. Tumetoa pia mapendekezo kuhusu fedha za umma na jinsi ambavyo fedha hizi zitaweza kulindwa. Tumependekeza kwamba Bunge iwe ndio msimamizi wa fedha hizi na kwamba fedha ambazo hazijaidhinishwa na Bunge zisitumike na pia jinsi ambavyo serikali itaweza kuomba mkopo, either ni hapa nchini ama ni nchi za kigeni.

Tumependekeza pia shughuli za Banki Kuu ya Kenya, pia tumegawanisha ofisi ya msimamizi wa fedha za umma. Tumependekeza tuwe na Controller of budget au atakaye simamia makisio ya fedha za umma na kuhakikisha kwamba fedha zinazotengwa zimetumiwa kwa njia iliyoidhinishwa na Bunge. Halafu tukapendekeza tuwe na Auditor General ambayo ni mkaguzi mkuu wa fedha za umma atakaye simamia na kuhakikisha kwamba hizo fedha zilitumika kwa njia iliyo ya haki.

Halafu tumetazama katika chapter ya kumi na nne, huduma za umma public service na tukapendekeza msimamo unaofaa kuchukuliwa na wafanyikazi wa umma, Article 258. Na tukapendekeza kwamba wafanyikazi wote wa umma ni lazima wawe wanafanya kazi yao kwa hali ya juu. Ni lazima pia wafanye kazi yao ambayo ni ya usawa katika uchumi wetu. Ni lazima wafanye kazo yao kwa njia ya haki. Ni lazima pia wajishughulishe na misimamo ya kitaifa na ya kisekali. Wawe wanatumikia wanannchi kwa hali ya haraka. Wawe na uwazi katika shughuli zao. Wawe na uwajibikishaji katika kazi zao. Waandikwe kwa sababu wamestahili kuandikwa, na sio kwa mapendeleo na wawe wanapewa training mara kwa mara na pia katika uandikishaji wa watu katika sector hii ya umma, kuangaliwe kwamba kuna usawa wa wake na waume na watyu wasibaguliwe kupitia kabila zao. Na tukaweka Tume ya huduma ya umma na tukaipatia kazi ambayo watafanya. Mtasoma na kuelewa kazi ambayo Tume hii itakayokuwa inafanya.

Kisha tukaangalia sector ambayo ni ya huduma ya usalama. Na katika sector hii tumesema na kupendekeza kwamba zitambuliwe katika Katiba kwa sababu katika Katiba ya wakati huu, huduma za usalama ingawa ni muhimu hazikutabulikana. Na tukapendekeza sector zifuatazo polisi, wa utawala, jeshi la ulinzi, jeshi la wanamaji, jesho la wanahewa na kikosi cha upelelezi. Na pia sisi tukaziwekea na kupendekeza kanuni watazo fuata. Kwa mfano, tumependekeza kwamba wasifungamane na pande zozote za kisiasa, wawe na udhibiti kwa raia, waheshimu kanuni za sheria, demokrasiaa na haki za kibinadamu. Wawe na uwazi na iwajibikaji katika kazi yao. Waongozwe na sheria, wasitii amri isiyo ya kisheria na wasijiuzishe na vitendo visivyoleta manuufaa ya kiuchumi. Walinde uhuru wa wananchi na kusaidia wakati wa shida na wawe na nidhamu ya hali ya juu na uzalendo kwa nchi yetu.

Jambo lingine pengine mngepanda kujua ni kwamba katika huduma ya magereza, tumependekeza kubadilisha jina la huduma hiyo na kuiita Kanya Correctional Services. Kwa sababu huduma ambayo inafaa kutolewa na magereza ni kujaribu kuwabadilisha wahalifu ili wakifika katika jamii baada ya vifungo vyao wawe ni watu ambao wanaweza kuwa na manufaa katika jamii. Na tukaona pengine jina likibadalishwa litaweza kuwa na manufaa katika huduma hiyo.

Katika chapter ya kumi na tano, tumependekeza kuwa na National Security Council itakayo simamia huduma ya usalama na tukatoa shughuli zake na watakao kaa pale. Na pia tukaomba kuwe na huduma ya utawala na tukapendekeza kazi watakayofanya na watakao kaa pale.

Katika chapter ya kumi na sita, kuna Leadership and Integrity, yaani ni mambo gani watakayo zingatia viongozi. Majukumu yao pia tumeyaweka hapo mtaweza kusoma.

Chapter ya kumi na saba, tumeangalia chombo tunachosema kiwe ni chombo cha nne katika serikali na hizi tunaziita vyombo vya Kikatiba. Na tumependekeza tuwe na vyombo kadhaa. Tumesema tuwe na Tume mbali mbali zitazosimamia huduma kama vile huduma ya umma, huduma ya mahakama, huduma ya Bunge. Halafu pia tumependekeza tuwe na Tume ya Haki za Kibinadamu na haki za kitawala. The Commission on Human Rights and Administrative Justice. Tumependekeza tuwe na Tume ya maadili ya uhaminifu, Ethics and Integrity Commission. Tumependekeza tuwe na Tume ya uchaguzi, Electoral Commission, tumependekeza tuwe na kamati au Tume ya mishahara na malipo, Salaries and Remuneration Commission. Tumependekeza tuwe na Tume ya Katiba, Constitutional Commission, tumependekeza pia tuwe na Judicial Service Commission. Tumependekeza pia tuwe na Public Service Commission. Tumependekeza pia tuwe na Public Service Commission, tumependekeza pia kama chombo cha Kikatiba ofisi ya Mkuu wa Sheria. Mkurugezi wa mashtaka, Deputy Public Prosecutor, Public Defender ambaye ni wakili wa umma. Na kama nilivyosema Govenor wa Banki Kuu na msimamizi wa makadilio ya mapato na matumizi wa fedha. Mhasibu Mkuu wa ofisi ya kitaifa ya uhasibu Auditor General na pia Tume ya ardhi. Mkisoma mtaona kwamba hizi Tume tumezipatia kazi zitazokuwa zinafanya ili kuhakisha kwamba tuna utawala ulio bora.

Katika chapter ya kumi na tisa, tumeangalia jinsi tutaweza kubadilisha Katiba. Na tumependekeza kwamba kwa wakati huu

Katiba ibadilishwe kwa njia ifuatayo. Kwamba kukiwa na miswada ya kubadilisha Katiba katika kutengeza sheria Bunge huwa na readings ama msomo mara tatu. Kwamba, katika second and third reading ni lazima kupitishwe by two-thirds majority ya wanachama wote wa Bunge. Lakini pia tumependekeza kwamba, sio Katiba mzima iwe inapitishwa na two-thirds majority. Kwamba mambo yafuatayo yapitishwe na kuletwa kwa kura ya maoni ipingwe na wananchi, na jukumu ambalo limepewa wananchi wa kawaida katika Katiba.

